IMANI BILA MATENDO IMEKUFA
(Yak 2:17)

Imetukuta Kwaresima nyingine kama mwaka juzi na mwaka jana. Ni siku arobaini zingine za fursa ya neema. Kumbe kweli tunapewa neema juu ya neema (Yn 1:16). Kwaresima ni fursa ya kujipatanisha na Mungu na wenzetu pia. Majaliwa haya ni kwa sababu Mungu hataki tufe katika hali mbaya, bali anatupatia fursa zote hizo kusudi sote tuifikie toba (1 Pet 3:9).
Kumbe, usikubali katu kauli ya kwamba mtu ataokoka kwa imani tu. Kauli hiyo ilikuwa tikitaka ya Martin Luther tu. Usimpinge Yesu Kristo pamoja na Maandiko Matakatifu kinyemela. Kama ingelikuwa hivyo Yesu asingelisema na kufundisha mambo mengi sana. Nakupa mifano. Yesu asingalisema, "Mtu yeyote atakayeyafanya mapenzi ya Mungu, huyo ndiye ndugu yangu, na umbu langu, na mama yangu (Mk 3:35).
Wala asingalisema, "Si kila mtu aniambiaye Bwana, Bwana atakayeingia katika ufalme wa mbinguni, bali yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni…. Kila asikiaye hayo maneno yangu na kuyafanya, atafananishwa na mtu mwenye akili, aliyejenga nyumba yake juu ya mwamba…. Na kila asikiaye hayo maneno yangu asiyafanye, atafananishwa na mtu mpumbavu, aliyejenga nyumba yake juu ya mchanga" (Mt 7:21. 24.26).
Wala asingelitoa mfano wa watenda kazi waliofanya kazi kwenye shamba la mizabibu wakalipwa dinari baada ya kazi (Mt 20:1-16). Tena asingeliuadhibu ule mtini ambao ulisheheni majani mazuri lakini pasipo matunda (Mk 11:12-14).
Zaidi ya hayo, asingalitoa mfano wa watu walipewa talanta, wale waliowekeza na kuzalisha faida wakasifiwa na kupewa tuzo kinyume na yule ambaye aliificha talanta yake kwenye kitambaa akalaumiwa na kuadhibiwa (Lk 19:12-27). Hatimaye, asingelitulinganisha wanadamu na mtini tasa ambao mtunza bustani ameuombea muda wa kuupalilia na kuutilia samadi ili ukatwe vizuri ikiwa hautazaa matunda baada ya jitihada zote hizo (Lk 13:6-9).

Matendo ni Muhtasari wa Amri ya Mapendo

Kwaresima tutahimizana tukiambiana tuongeze matendo ya kusali, kufunga na kutoa sadaka (Mt 6). Lakini matendo haya matatu yaliyo nguzo za matendo katika Kwaresima ni muhtasari tu wa amri mpya ya mapendo. Hata hivyo, upendo uko pacha: upendo kwa Mungu na upendo kwa jirani. Kumbe sasa hebu tutazame kirefu kidogo jambo hili.

1. Kumpenda Mungu

Wakristo hatuna budi kuanza na kumpenda Mungu na kumpenda Mungu ni katika mambo matano makubwa yafuatayo: kumwabudu, kusali, kutoa sadaka na zaka, kumwekea ahadi au nadhiri na kuzitimiza na toba.

Kumwabudu Mungu: Wakristo tumwabudu Mungu. Tutenge muda wa kumsujudia Mungu. Kumwabudu Mungu ni kama "kumpa Mungu shikamoo yake". Tumpe. Mungu ni roho,

tumwabudu rohoni (Yn 4:23-24). Tusimfanyie tadi na inda. Tushike kitakatifu siku ya Mungu na tunapowahimiza watu wamwabudu Mungu sisi nasi tuwemo ndani. Tusiwe wasemaji na makocha wa nje tu. Tukiwa makocha tuwe "makocha - wachezaji".

Kusali: Maadhimisho ya misa yaendelee, kwa ubora zaidi, KUWA KIINI CHA MAISHA yetu ya kiroho. Tunakumbushana tusali. Tuwamo katika sala. Hata hivyo tunaposali tuitunze nidhamu aliyoitaka Yesu Kristo, tusibwatebwate kama watu wasiomjua Mungu (Mt 6:5-11). Tusimpinge Kristo Yesu. tusiwe wapinga Kristo (Mt 7:21-23, Mk 3:31-34). Kauli yake i wazi kabisa. Kusali kwa kupayukapayuka ni dalili ya matatizo matano: kutokujua Mungu alipo, kutokuwa na heshima, kutokukua, kuwa na shida kubwa moyoni na kukosa subira. Waaidha,katika kusali, wala tusimfanyie Mungu fujo kwa sekeseke la kukamia kunena lugha ngeni na kutoa unabii. Kuna amri ya kukataza fujo hii katika 1Kor 14:1-40. Tusipinge amri ya Yesu aliyotupatia kwa kinywa cha Mtume Paulo (1Kor 14:37-38).

Kutoa sadaka na zaka: Jambo lingine ni kutoa sadaka na zaka ili kazi ya Uinjilishaji iendelee. Sadaka haina kiwango ni kadiri ya moyo wetu tu, lakini zaka ni moja ya kumi ya mapato yetu ya mwaka. Tumtolee Mungu sadaka na zaka kwa ajili ya kueneza ufalme wake, kulijenga na kuliimarisha Kanisa na kulipa uwezo wa kuwahudumia wenye dhiki. Tusimwibie Mungu (Mal 3:8) na tunaambiwa ni heri kutoa kuliko kupokea (Mdo 20:34-35).

Kumwekea Mungu ahadi na nadhiri na kuzitimiza: Jambo lingine ni kumwekea Mungu ahadi au nadhiri na kuzitimiza. Sisi ni watu wa ahadi. Wakristo tumemwekea Mungu ahadi nyingi: za ubatizo, za ndoa, za kitawa, za kipadre na kadhalika. Wasiofunga ndoa hawajawekeana ahadi za kweli wanataka siku yoyote wakimbiane. Wanadanganyana ndiyo maana wanaoogopa kufunga ndoa. Lakini, kama tumeweka ahadi tujue tuna deni maana ahadi ni deni na dawa ya deni ni kulipa.

Kufanya toba: Jambo la mwisho katika kumpenda Mungu ni toba. Wakristo tufanye toba. Mzee Yoshua ben Sira anatuasa tusichelewe kuungama dhambi zetu akisema: "Usiseme, 'Nimetenda dhambi, lakini nimepata balaa gani?' maana Bwana hakasiriki upesi. Usitegemee kupata msamaha hata kuongeza dhambi juu ya dhambi. Usiseme, 'Huruma yake ni kubwa; yeye atanisamehe dhambi zangu nyingi.' Kumbuka, yeye ana huruma na ghadhabu na hasira yake huwakumba wenye dhambi. Usichelewe kumrudia Bwana, wala usighairishe kurudi siku hata siku. Maana ghadhabu ya Bwana itakuwakia ghafla, na wakati wa hukumu utaangamia" (YbS 5:4-7).
Na mahali pengine anasema, "Usivutwe kutenda dhambi mara mbili, maana hutaacha kuadhibiwa hata kwa moja. Usiseme, 'Mungu atapokea wingi wa sadaka zangu, nikimtolea Mungu Mkuu dhabihu lazima atapokea.' Usisitesite katika sala, wala usisahau kuwapa masikini sadaka" (7:8-10).

2. Kumpenda Jirani – Matendo 14 ya Huruma

Baada ya kumtendea Mungu matendo ya upendo, tunapaswa kutendeana matendo ya upendo sisi kwa sisi. La sivyo, tutakuwa waongo kabisa. Yaani tutakuwa watu wenye utapiamlo wa upendo wa kweli. Tazama tumeandikiwa hivi, “Mtu akisema kwamba anampenda Mungu, hali anamchukia ndugu yake, huyo ni mwongo. Maana mtu asiyempenda ndugu yake ambaye anamwona, hawezi kumpenda Mungu ambaye hamwoni. Basi, hii ndiyo amri aliyotupa Kristo: Anayempenda Mungu anapaswa pia kumpenda ndugu yake” (1Yn 4: 20-21).

Matendo Saba ya Huruma ya Kimwili *(rejea Mt 25:31-45)*
Matendo hayo ni: kuwalisha wenye njaa, kuwanywesha wenye kiu, kuwavika wasio na nguo, kuwakaribisha wageni, kuuwatembelea wagonjwa, kuwatembelea wafungwa na kuwazika wafu.

Matendo Saba ya Huruma ya Kiroho
Matendo hayo ni: kuwafundisha wajinga (wasiojua), kuwashauri wenye mashaka, kuwafariji wenye dhiki, kuwaonya wakosefu, kusamehe (kuvumilia) makosa, kuwavumilia wasumbufu na kuwaombea wazima na wafu.

Shime ndugu zanguni. Hakika tukifaulu kuyatenda matendo yale matano kumwelekea Mungu pamoja pamoja na haya kumi na manne kuwaelekea majirani zetu hatutagaa gaa na upwa tukala wali mkavu bali tutakaribishwa mbinguni na kumwagilia moyo. Ndipo tutakuwa tumechumia juani na kulia kivulini.
Basi, Kwaresima ndiyo hiyo tuhimizane na tujihimize katika haya yote kusudi Pasaka ya duniani hapa sawia na ile ya mbinguni zitukute “kamili gado.” Imani bila matendo imekufa na matendo bila imani ni kazi bure.